# Makubaliano ya Mtumiaji wa Kifaa cha Muunganisho wa Intaneti ya Digital Dreamers kwa SY2024 – 2025

Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb itatoa Kifaa cha Muunganisho wa Intaneti kwa familia za wanafunzi katika gredi za PreK – 12 ili kutumiwa wakati wa mwaka wa masomo (SY 2024 – 2025). Vifaa vya Muunganisho wa Intaneti vitasalia kuwa mali ya DCSD (Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb), na lazima virejeshwe baada ya kuchukuliwa kutoka kwa wilaya na/au wakati wa mchakato wa ukusanyaji wa mwisho wa mwaka.

Wazazi na wanafunzi wanahitajika kusoma, kutia saini na kufuata maelekezo yaliyo katika hati hii, na pia sera na taratibu za shule, darasani na Wilaya ya Shule kuhusu tabia na matumizi ya teknolojia.

**Mtu wa kuwasiliana naye:** Ikiwa una maswali au wasiwasi tafadhali wasiliana na usimamizi wa shule yako.

## Makubaliano ya Mtumiaji wa Kifaa cha Muunganisho wa Intaneti

**Kupokea Kifaa**

Lazima wazazi na wanafunzi watie saini na warejeshe makubaliano haya kabla ya kifaa kupeanwa.

**Kurejesha Kifaa**

Vifaa vitarejeshwa shuleni mwisho wa mwaka wa masomo. Matumizi ya vifaa vinavyotolewa na DCSD hayawezi kuhamishwa kwa mtu mwingine na hukoma wakati mwanafunzi amekoma kuwa mwanafunzi wa shule inayotoa kifaa.

Wanafunzi wanaohama, kuondoka, kufukuzwa au kukoma kuwa wanafunzi kwa sababu yoyote ile lazima warejeshe vifaa vyao siku ya kujiondoa/kukoma kuwa wanafunzi.

Mwanafunzi yeyote anayekosa kurejesha kifaa atalazimika kulipia gharama kamili ya kubadilisha vifaa na vifuasi vyovyote, na huenda pia kadi za gredi, nakala za alama, diploma, au vyeti vyake vya maendeleo vikachukuliwa hadi gharama hiyo ilipwe.

**Hasara na Upotezaji**

Ikiwa kifaa kimeharibika, kimepotea au kuibiwa wakati ambao kinatumika na mwanafunzi aliyepewa, iwe kimakusudi au kwa sababu ya uzembe, mwanafunzi na mzazi/mlezi wa mwanafunzi watawajibika kwa faini zilizowekwa katika hati hii.

**Utelekezaji**

Usimamizi wa wilaya utaamua hatua itakayochukuliwa ikiwa ni pamoja na kulipia kamili ubadilishaji wa Kifaa cha Muunganisho wa Intaneti ikiwa kifaa kimeharibika mara nyingi katika mwaka sawa wa masomo.

**Matumizi Mema ya Kifaa**

Watumiaji wote wa vifaa vinavyotolewa na Wilaya lazima wakidhi matarajio yaliyobainishwa katika Sera ya Wilaya na Mwongozo wa Uendeshaji wa *IFBGA: Matumizi Yaliyowajibika ya Mtandao wa Biashara, JD: Nidhamu ya Mwanafunzi/Kanuni ya Maadili Mema ya Wanafunzi,* na *JS*: *Faini, Ada na Gharama za Wanafunzi.* Kushindwa kufuata matarajio haya kutasababisha kuchukuliwa kwa hatua za kinidhamu kwa mwanafunzi husika. Sera zote za Wilaya zinaweza kupatikana katika www.dekalbschoolsga.org.

Vifaa hivi vimewekwa vizuizi Vinavyotii Sheria ya CIPA (Sheria ya Intaneti ya Ulinzi wa Watoto) na wilaya ya shule na vinapaswa kutumika kwa madhumuni ya mafundisho pekee. Wanafunzi wanapokuwa nje ya maeneo ya shule, wazazi/walezi watawajibika kufuatilia wanafunzi wanavyotumia kifaa. Wanafunzi hawaruhusiwi kuonyesha tabia zisizofaa, au kufikia nyenzo zisizoruhusiwa kwa kutumia kifaa hiki, wakati wowote ule, katika eneo lolote lile. Wanafunzi wanaweza kuchukuliwa hatua ni kinidhamu na/au za kisheria ikiwa watatumia kifaa kwa shughuli zisizofaa, iwe ndani au nje ya maeneo ya shule.

**Faragha**

Vifaa vinavyotolewa na wilaya vitasalia kuwa mali ya DCSD. Kwa hivyo, kitu chochote kinachofanywa kwenye kifaa si cha faragha. Hii inamaanisha wahudumu wa DCSD wanaweza, wakati wowote ule, kuchukua na kutafuta matumizi yoyote ya kifaa cha kielektroniki kilichotolewa na Wilaya.

Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb inatambua vipengele vyote vya Sheria ya Mtandaoni ya Ulinzi wa Faragha ya Watoto (**COPPA**), Sheria ya Intaneti ya Ulinzi wa Watoto (**CIPA**), na Sheria ya Faragha na Haki za Elimu ya Familia (**FERPA**).

Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb haifuatilii mitandao, vifaa na muunganisho wa intaneti katika nyumbani kwa mwanafunzi. Wilaya haifuatilii matumizi ya vifaa vinavyotolewa na Wilaya. Aidha, DCSD inafuatilia eneo la vifaa vinavyotolewa na Wilaya katika tukio la wizi au kupotea.

**Matumizi ya Vifaa ya Kila Mwezi**

Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb inafuatilia matumizi ya kifaa kila mwezi. Ikiwa wilaya itagundua matumizi madogo, wilaya itawasiliana na wazazi ili kuona ni aina gani ya msaada unaoweza kutolewa. Wilaya ina haki ya kuomba familia irudishe kifaa ikiwa kifaa kinatumiwa kidogo sana au ikiwa kuna ukiukaji wa Makubaliano ya Matumizi Yanayokubalika.

**Faini za Kuharibu, Kupoteza au Kuibiwa kwa Kifaa**

Ikiwa kwa sababu yoyote ile kifaa au vifuasi vimepotea au kuibiwa wakati vinatumiwa na mwanafunzi, iwe kimakusudi au kwa sababu ya uzembe, mwanafunzi na mzazi/mlezi watawajibika kwa faini zifuatazo:

**Kubadilisha Kifaa cha Muunganisho wa Intaneti**

| | |
|---|---|
| **Kupotea/Kuibiwa/Kuharibika hadi hakiwezi Kutengenezwa** | • Ada kamili ya kubadilisha ($90.00 kulingana na kifaa kinachopatikana kwa ununuzi) |
| **Kimeharibika lakini kinaweza Kutengenezwa** | • Vifaa vilivyoharibika vitachunguzwa na timu ya DCSD ili kubaini ikiwa vinaweza kutengenezwa. Ikiwa kimeharibika hadi hakiwezi kutengenezwa ada kamili ya kubadilisha itahitajika. Angalia hapo juu. |

**Gharama kamili ya kubadilisha vifaa hujumuisha kifaa, vifuasi vyake vyote, leseni za programu na kuweka programu.*

**Wizi:**

Ikiwa kifaa kimeibiwa wakati kinatumika na mwanafunzi, mwanafunzi na mzazi/mlezi watawajibika:

- Kuarifu Usimamizi wa Shule
- Kuandikisha ripoti kwa polisi
- Kulipia ada kamili ya kubadilisha kifaa

**Kukosa Kurejesha Kifaa au Vifuasi baada ya Kuhama/Kuondoka Shuleni:**

Mwanafunzi anayehama au kuondoka na kukosa kurejesha kifaa au vifuasi vyovyote atawajibika kwa ada kamili ya kubadilisha Kifaa cha Muunganisho wa Intaneti.

## KIBALI NA IDHINI YA MZAZI

Kwa kutia saini hapa makubaliano haya, unaashiria kwamba umesoma na kuelewa maelekezo katika hati hii na umekubali mwanafunzi wako kupewa kifaa. Unaelewa kuwa Kifaa cha Muunganisho wa Intaneti kinasalia kuwa mali ya DCSD na lazima kirudishwe baada ya kuondoka kwenye Wilaya na/au wakati wa mchakato wa ukusanyaji wa mwisho wa mwaka. Unaelewa kwamba mwanafunzi wako anawajibika kwa uharibifu, upotezaji au wizi wa kifaa na vifuasi wakati anavitumia na anakubali faini zilizo katika hati hii.

Unaelewa na kukubali kwamba, akiwa nje ya maeneo ya shule, unawajibika kufuatilia jinsi mwanafunzi anavyotumia kifaa na kifaa hicho kinapaswa kutumiwa kwa malengo ya mafundisho PEKEE. Unaelewa kwamba wanafunzi wanaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa watatumia kifaa kwa shughuli zisizofaa au zilizokatazwa.

Wewe na mwanafunzi wako mnakubali kuwa Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb haitawajibika kwa uharibifu wa kimakusudi au usio wa kimakusudi unaotokana na matumizi mabaya, matumizi yasiyofaa, ubadilishaji, udukuzi au uharibifu wa vifaa. Mtumiaji yeyote mwanafunzi asiyetii Matumizi Yanayokubalika ya Intaneti ya Wilaya ya Shule za DeKalb, ataweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu zilizowekwa na usimamizi wa shule yake. Makosa ya mwanafunzi yanaweza pia kusababisha kuchukuliwa kwa hatua zinazofaa za kinidhamu kwa kuongezea kusitishwa au kuondolewa kwa uwezo wa ufikiaji.

**Jina la Mzazi/Mlezi**

**(Tafadhali Andika):** ______________________________________________

**Mzazi/Mlezi**

**Saini:** ________________________________________________________ Tarehe: __________

## MAKUBALIANO NA SAINI YA MWANAFUNZI

1. Nitatunza vizuri kifaa nilichopewa na shule yangu.
    a. Lazima nyaya na kebo ziingizwe kwa makini kwenye kifaa ili kuzuia uharibifu.
    b. Vifaa havipaswi kamwe kuachwa kwenye kabati au gari ambalo halijafungwa au eneo lolote lisilochungwa.
    c. Ripoti matatizo yoyote ya programu/maunzi kupitia Incident IQ- Kituo cha Usaidizi cha Wanafunzi.
    d. Hakikisha kifaa kimelindwa vizuri na kiko katika mazingira ambayo halijoto imedhibitiwa wakati hakitumiki.
2. Sitawahi kupeana kifaa changu nilichopewa na shule yangu kwa watu wengine.
3. Nitaweka vyakula na vinywaji mbali na kifaa changu.
4. Sitafungua, kuondoa vizuizi au kudukua kwenye sehemu yoyote ya kifaa changu au kifaa chochote nilichopewa na shule.
5. **SITAJARIBU** kufanya matengenezo kwenye kifaa changu.
6. Nitalinda kifaa changu nilichopewa na shule kwa kukibeba katika mfuko wake niliopewa.
7. Nitatumia kifaa changu nilichopewa na shule kwa njia ambayo inafaa na inatimiza matarajio ya shule - iwe shuleni, nyumbani, au mahali pengine. Ikiwa nitatumia kifaa changu kwa njia isiyofaa, ninaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu na shule yangu.
8. **SITABANDIKA** mapambo (kama vile vibandiko, alama, nk.) kwenye kifaa nilichopewa na shule. Sitaharibu kibandiko cha nambari tambulishi kwenye kifaa nilichopewa na shule.
9. Ninaelewa kwamba kifaa changu nilichopewa na shule kinaweza kukaguliwa wakati wowote bila taarifa. **HAKUNA chochote ninachokifanya au kiko kwenye kifaa ni cha faragha.**
10. Sitashiriki manenosiri yangu na mtu mwingine isipokuwa mwalimu au mtu mzima kutoka shule yangu au mzazi/mlezi wangu.
11. Ninaelewa kuwa Kifaa cha Muunganisho wa Intaneti kinasalia kuwa mali ya DCSD na lazima kirudishwe baada ya kuondoka kwenye wilaya na/au mwisho wa mwaka wa masomo wakati wa mchakato wa ukusanyaji.
12. Ninaelewa kwamba nikiharibu au kupoteza kifaa changu, au kiibiwe, nitalazimika kulipia gharama ya kubadilisha kifaa.

**Ninakubali kanuni zilizobainishwa katika Makubaliano ya Mtumiaji wa Kifaa na Makubaliano ya Mwanafunzi.**

**Jina la Mwanafunzi (Tafadhali Andika):** ______________________________

**Saini ya Mwanafunzi:** ________________________________________ Tarehe: __________